

Mission: Majibu ya Insha zetu (Nov 2005) kuhusu swala ya Ukuaji wa AIC(T) Pwani.

1. Kanisa kwa jumla

Vikwazo vinyovizua kanisa la AIC lisikue ni kwamba kanisa limeshikilia sana msimamo wa kwanza kwa kanisa, yaani jinsi ilivyoanza, halitaki kubadilika kulingana na mabadiliko ya Ulimwengu wa sasa. (Kwa mfano , kuwaombea wagonjwa na watu ambao wanao mapepo)

- a) Uhaba wa mafundisho.
 - b) Kikwazo kingine ambacho kinasababisha kanisa la AIC(T) lisingezeke ni jinsi kanisa la AIC linavyojulikana na watu wengi, linaitwa kwamba ni kanisa la Wasukuma. Wakristo wa AICT wamefungwa na mila ya wasukuma kiasi kuwa kila wanaopkwenda kuanzisha kanisa wanalazimika kufuta utaratibu na mila za kisukuma hata kama si mahali pa Wasukuma.
 - c) Ukosefu wa maono na mipango kwa viongozi na ngazi zote.
 - d) Kanisa linajali rika na mafunzo badala ya vipawa na uwezo.
 - e) Hakuna nafasi ya kuzungumzia mipango au mikakati ya kuwatafuta waliopotea.
 - f) Kutotilia maanani lengo au kipaumbele cha Mungu kwa Kanisa lake. Matt 28:19-20. Karibu na asilimia 95% ya mapato yanafanya kazi za maendeleo ya kawaida.
 - g) Kazi ya kupeleka Injili kwa wasioamini ni ya wamisionari wageni. 'Mzungu mwenye pesa'.
 - h) Kazi ya upandaji makanisa nje ya mipaka ya AICT inakuwa ngumo mno.
 - i) AICT limeacha kujihusisha na huduma za ki-jamii.
 - j) Umsihenari kanisani umo katika makaratasi si kwa matendo. ukosefu wa maandalizi.
 - k) Hakuna walioandaliwa kuwahudumia wamishenari.
2. **Wazee na wahudumu** wa kanisa nao wanakuwa ni kikwazo badhi yao kwa sababu ya ushuhuda wao unakuwa siyo mzuri ndani ya kanisa na baadhi yao wanaona ni sifa kuitwa mzee wa kanisa lakini hawako tayari kutumuka kwa moyo wote na kujitoa kwa sababu ya ushuhuda kuwa mbaya.

3. Wachungaji/Wainjilisti

- a) Kutopata mahitaji yao ya mwili-vizuri
- b) Uhamisho na Utumaji
- c) Dhana mbovu ya Baadhi ya watumishi kujipatia ukuhani.
- d) Kutotiana moyo katika watumishi
- e) Dhana mbvu ya kuridhika na hali duni
- f) Kukosa uaminifu katika Utendaji.
- g) Kutokuvitumia vipawa na vipaji walivyo nadani ya local church.
- h) Kuto kucombeana, kutembeleana, kutaina moyo.
- i) Kutegemea local church au pastoreti kwa posho.
- j) Viongozi wengi wa Kanisa wanaingia kazini kwa ajili ya uchu wa madaraka na kutaka vyeo na kuonekana kuna ni Wachungaji tu.
- k) Hawana mipango maalum wa upandaji wa maeneo ambayo hayajafikiwa na Injili.
- l) Hawatafanyi elimu ya ufuasi.

4. Local church

- a) Kutopewa uhuru wa kujijendesha kulingana na mahitaji yake.
- b) Umoja katika kazi ya Bwana na hata mwili wa Kristo.
- c) Kutoiga na kutoshirikiana na makanisa/ madhehebu yanayohubiri Injili ya kweli.
- d) Kutokuwa na maombi ya kudumu/kukata tamaa.
- e) Wakristo wa AICT hawapendi kujifunza neno la Mungu kwa kigezo. Wanajiona wamekamilika hawahitaji mafundisho mengine. Siku za mafundisho wanakuwa hawana nafasi. Kwa kifupi ni kwamba hawajali mafundisho na kwa upofu wa roho hawoni faida ya mafundisho.
- f) Kutojija mipango ya shetani katika Ulimwengu wa Roho.
- g) Hakuna mwamko wa kufanya mikutano ya Injili ya nje. Inafanyaika mara chache.

- h) Ushuhuda mbaya wa kanisa mahali lilipo.
- i) Wakristo wengi ni wachanga kiroho.
- j) Kuna watu ambao ni Wakristo wa jina tu! Wamezaliwa kanisani.
- k) Mapokeo : ukarimu kwa wageni wanaotutembelea na wanaosimima kanisanani.
- l) Kuna umbali mrefu toka Mchungaji na Waumini. Hasa katika makanisa makubwa.
- m) Kanisa linapaswa kufundishwa na kujua juu ya mission, na missionary ni nani na majukumu yake ni nini?
- n) Hakuna elimu ya ufuasi.
- o) Waumini wa AICT wanaamini kwamba Kazi ya kueneza Injili na kupanda makanisa ni kazi ya Mchungai tu. Siyo kazi zao.